Wekeza na jenga maisha na SACCOS

LESA SACCOS LTD

REG. No DSR 1299

SERA YA MLAJI

WEKA AKIBA MARA KWA MARA, KOPA KWA BUSARA LIPA KWA WAKATI, WEKEZA KWA MAENDELEO YAKO.

TOLEO LA I: 2020

UIDHINISHAJI WA SERA YA MLAJI

Tarehe ya Kupitishwa na Kikao Cha Bodi		**Kikao Cha Bodi Tarehe 17 Julai 2020**
Mpya **Imehuishwa**	☐ ☐	**Toleo la; I Mwaka 2020**

Imetiwa Saini kwa Niaba ya Wanachama na;

S/N	Jina	Wadhifa	Tarehe	Sahihi
1	EVA .J.BOSCO	Mwenyekiti wa Bodi	23/11/2020	[signature]
2	GWAMAKA JAPHARI	Mjumbe wa Bodi	23/11/2020	[signature]
3	SEMALY KISAMO	Mjumbe wa Bodi	23/11/2020	[signature]
4	SHAFII MMILE	Mjumbe wa Bodi	23/11/2020	[signature]
5	NAOMI SERBANTEZ	Mjumbe wa Bodi		

Imetiwa Saini kwa Niaba ya Watendaji na:

Jina	Wadhifa	Tarehe	Sahihi
DEONATUS KIHEKA	Meneja	28/09/2020	[signature]

Kwa Matumizi ya Mrajis:

Maoni ya Mrajis:

Jina	Wadhifa	Tarehe	Sahihi

Muhuri

YALIYOMO

UTANGULIZI 1
SEHEMU YA KWANZA 2
1.0 MISINGI YA SERA 2
1.1. Madhumuni ya Sera 2
1.2. Mambo Muhimu ya Kuzingatia 2
1.3. Walengwa wa Sera 2
1.4. Wajibu wa Mwanachama 3
1.5. Haki za Mwanachama 4
1.6. Wajibu wa Bodi na Watendaji wa Chama 4
SEHEMU YA PILI 6
2.0 HUDUMA ZITOLEWAZO NA CHAMA NA TARATIBU ZAKE 6
2.1 Huduma zitakazotolewa na Chama 6
2.2 Ubora wa Viwango vya Huduma 6
2.3 Utaratibu wa kutoa huduma 6
2.4 Ufuatiliaji wa Malalamiko 7
2.5 Jinsi ya kutuma Malalamiko au Mapendekezo 7
SEHEMU YA TATU 8
3.0 TAARIFA ZITAKAZOWEKWA WAZI WAKATI WOTE NA CHAMA 8
3.1 Taarifa zinazohusu Hisa, Akiba na Amana 8
3.2 Taarifa kuhusu Akaunti zenye Riba 8
3.3 Taarifa kuhusu Mabadiliko ya Masharti ya Akaunti 9
3.4 Taarifa ya Kipindi cha Huruma (*Grace period*) cha Kurejesha Mkopo 9
3.5 Taarifa kuhusu Mikopo 9
3.6 Taarifa kuhusu Sababu za Kukataliwa kupewa Mkopo 10
3.7 Taarifa kwa Wadhamini wa Mikopo 10
HITIMISHO .... Error! Bookmark not defined.

UTANGULIZI

LESA SACCOS LTD ilianzishwa kwa kuzingatia Sheria ya Vyama Vya ushirika Na.20 ya mwaka 2003.Kwa malengo ya kupokea akiba na kutoa Mikopo yenye masharti nafuu kwa wamanachama wake. Mkutano mkuu wa wanachama ndicho chombo cha juu chenye mamlaka katika shughuli zote za chama na kwa kuzingatia Sheria ya Vyama Vya ushirika Na. 6 ya mwaka 2013 kinatambua kuwa bodi ya chama ndio chombo pekee cha kuongoza chama kwa kuzingatia ukasimishwaji wa madaraka hayo kupitia mkutano mkuu wa wanachama.

Kifungu Na.52 cha Sheria ya Vyama Vya Ushirika kinaenda mbali zaidi na kutoa nafasi kwa bodi kuandaa miongozo mbalimbali ya kusimamia chama na miongoni mwa miongozo iliyotajwa ni pamoja na sera ya mlaji.

Sera hii imeweka mwongozo sahihi wa namna ya kumhudumia mteja ili kufanikisha lengo la Chama na mteja mwenyewe. Katika Kanuni ya SACCOS sehemu ya kumi na tano imeelezea taarifa muhimu ambazo mteja angependa kuzijua zinazotokana na huduma zitolewazo na Chama. Kwa kuzingatia Kanuni ya SACCOS na Sera hii, Bodi na menejimenti wakati wote itazingatia huduma Bora kwa maslahi ya Chama na wanachama na kuweka mikataba ya huduma.

Makubaliano ya mikataba ya huduma kwa wateja ni makubaliano ya ushirika kati ya Chama na wapokea huduma. Mikataba huanisha viwango vya huduma ambavyo Chama kinaamini walengwa wake watanufaika na huduma hizo. Vilevile, kuweka muundo wa ufuatiliaji na utatuzi wa matatizo pale yatakapojitokeza. Mikataba huandaliwa na bodi ya Chama kwa kuwashirikisha wateja.

Chama kimetambua umuhimu wa kutumia mikataba ya huduma kama chombo cha kuleta mabadiliko ya kiutendaji na kuleta mfumo wa huduma ambao unamlenga zaidi mteja. Ili sera hii iweze kufanya kazi inabidi iwe hai inayotokana na mahusiano mazuri ya kikazi yanayotarajiwa kujengwa ndani ya Chama kati ya Bodi, watumishi, wanachama pamoja na wadau wengine.

SEHEMU YA KWANZA

1.0 MISINGI YA SERA

1.1. Madhumuni ya Sera

Lengo la sera hii ni kukuza uelewa wa upatikanaji na ubora wa huduma zitolewazo na Chama. Hii itawezekana kwa kuwasaidia wanachama na wadau mbalimbali kuelewa shughuli za Chama, namna ya kuwasiliana na Chama, viwango vya huduma na jinsi ya kutatua matatizo yanapojitokeza. Sera hii itawasaidia walengwa kudai haki zao na kutekeleza wajibu wao na inatoa uwazi wa namna ya kuwasiliana na Chama kwa ajili ya kuwasilisha malalamiko.

1.2. Mambo Muhimu ya Kuzingatia

Katika kufanikisha azma ya utoaji huduma bora, ni wajibu wa Bodi ya Chama na watendaji kuzingatia mambo yafuatayo;

i. Kuelewa kwa undani kuhusu wateja na huduma ambazo ni muhimu kwao
ii. Taarifa za viwango vya huduma ambavyo wateja wanatarajia kupatiwa
iii. Mipango ya kutatua matatizo endapo yatajitokeza
iv. Maelezo mafupi ya namna ya kuwasiliana na kupata taarifa za Chama
v. Kuwajibika kwa mujibu wa Sheria ya Ushirika na Kanuni zake
vi. Kuwa na mpango wa kutoa elimu ya ushirika kwa wateja.
vii. Kuhakikisha kuwa, wateja wanashiriki vyema katika shughuli za Chama
viii. Kuimarisha uwezo na nguvu kazi ya Chama

1.3. Walengwa wa Sera

i. Wanachama wa LESA SACCOS.

Wanachama wa LESA SACCOS ndio wanufaika wakuu wa sera hii na hivyo wanatarajia yafuatayo:-

a) Kupata huduma iliyo bora
b) Haki ya kupata taarifa ya mwenendo wa Chama (Uwazi)
c) Kupata usawa wa jinsi katika uongozi
d) Kutatuliwa migogoro kati ya Chama na Wanachama

ii. Wahisani

Matarajio yao ni: -

a) Utawala Bora na wazi
b) Huduma za uhakika na;
c) Matumizi ya fedha za wahisani yanayokidhi haja.

iii. Tume ya Maendeleo ya Ushirika na Mkaguzi wa nje. Matarajio yao ni:-
a) Chama kutoa huduma bora na kwa wakati kwa wanachama wake
b) LESA SACCOS imara na yenye mafanikio kiuchumi kwa wanachama na Chama kwa ujumla
c) Huduma zitolewazo zizingatie zaidi mahitaji ya walengwa kuliko ya watoa huduma
d) Utawala na uratibu bora wa sera na mikakati mbalimbali ya kisekta
e) Uzingatiaji wa Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 mwaka 2013 na Kanuni zake.

iv. Watoa huduma ambao watapaswa kuzingatia mambo yafuatayo: -
a) Kujiepusha na vitisho vya kutumia nguvu au njia nyingine za jinai za kumdhuru, kumshushia hadhi au kuharibu mali za mwanachama yeyote;
b) Kutotumia lugha chafu;
c) Kutomshirikisha mtu yeyote katika mazungumzo kwa dhamira ya kuudhi, kutusi au kunyanyasa.
d) Mkusanya madeni hatapaswa kutumia uongo, udanganyifu au upotoshaji katika uwasilishaji kama njia ya kukusanya deni.
e) Vitisho vya kuchukua hatua zozote ambazo kisheria hataweza kuchukua au ambazo hazidhamiriwi kuchukuliwa

1.4. Wajibu wa Mwanachama

Mwanachama anapaswa kutekeleza mambo yafuatayo:-
a) Uzingatiaji wa Sheria, Kanuni za ushirika, masharti ya Chama, kanuni za maadili, kanuni za ndani, sera na taratibu za Chama
b) Kulipa ada, hisa na malipo mengine yoyote ya Chama
c) Kushiriki katika shughuli za kiuchumi za Chama kama inavyotakiwa katika masharti
d) Kuhudhuria mikutano
e) Kulipa madeni ya Chama

f) Kutekeleza maazimio ya Mkutano Mkuu
g) Kulinda na kutetea mali na maslahi ya Chama
h) Kuhifadhi na kulinda taswira na sifa za Chama
i) Kutekeleza wajibu wake kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Masharti ya Chama

1.5. Haki za Mwanachama

Pamoja na mwanachama kuwa na wajibu kama ilivyoelezwa hapo juu, pia ana haki zifuatazo:-

a) Kupiga na kupigiwa kura
b) Kuhudhuria na kushiriki katika mikutano ya Chama
c) Kushiriki katika uongozi wa Chama cha ushirika
d) Kuitisha Mkutano Mkuu maalum kwa mujibu wa sheria ya ushirika na masharti ya Chama
e) Kukopa kutoka kwenye Chama
f) Kumiliki hisa za Chama
g) Kutaarifiwa kuhusu masuala yote ya Chama
h) Kupokea gawio na faida nyingine kutoka katika shughuli za Chama
i) Kushiriki katika kutunga na kurekebisha masharti ya Chama
j) Kujitoa uanachama
k) Kuhoji kuhusu masuala ya Chama
l) Kukata rufaa kama ilivyo katika Sheria, Kanuni za ushirika na masharti ya Chama
m) Haki nyingine zozote zile ambazo Chama kinaweza kuweka, kwa vigezo vya masharti.

1.6. Wajibu wa Bodi na Watendaji wa Chama

Ili kufanikisha azima ya wanachama, bodi ya chama na watendaji watapaswa kuzingatia yafuatayo:-

i. Kuwa watii kwa Chama
ii. Kuwajibika ipasavyo katika kusimamia Chama
iii. Kutoa huduma bila upendeleo

iv. Kuheshimu Sheria Na.6 ya vyama vya ushirika ya mwaka 2013 na Kanuni zake

v. Matumizi bora ya taarifa za kikazi na;

vi. Uadilifu na uaminifu.

SEHEMU YA PILI

2.0 HUDUMA ZITOLEWAZO NA CHAMA NA TARATIBU ZAKE

2.1 Huduma zitakazotolewa na Chama

Chama kitatoa huduma zifuatazo kwa ajili ya wateja wake ambao ni Wanachama

i. Hisa za Uanachama: Chama kitakuwa na huduma ya kuweka hisa za lazima kwa ajili ya kujiunga na Chama. Taratibu za uwekaji hisa za lazima zimeaninishwa katika sera ya uhamasishaji wa Hisa, Akiba na Amana.

ii. Hisa za Hiari: Chama kitakuwa na huduma ya kuweka hisa ya hiari. Ili Mwanachama aweze kuweka hisa hizi Chama kitaweka riba itakayo mvutia Mwanachama. Taratibu za uwekaji hisa za hiari zimeaninishwa katika sera ya uhamasishaji uwekaji wa Hisa, Akiba na Amana.

iii. Mikopo: Chama kitatoa aina mbalimbali za mikopo kwa Wanachama wake kwa kuzingatia mahitaji halisi ya Mwanachama na vigezo na masharti ya Sera ya Mikopo ya Chama.

iv. Kutoa elimu ya Ushirika: Kila mara, Chama kitatoa elimu ya Ushirika kadri ya mapendekezo ya Wanachama. Elimu itatolewa kwa njia mbalimbali ikiwemo kupitia Mkutano Mkuu na njia nyingine Bodi itakazoona zinafaa.

2.2 Ubora wa Viwango vya Huduma

Chama kitatoa huduma kwa kuzingatia mambo yafuatatyo;

i. Uwajibikaji
ii. Matumizi ya lugha kwa ufasaha
iii. Kwa kuzingatia ushauri wa wanachama na wadau
iv. Kutoa huduma kutokana na mahitaji ya mwanachama

2.3 Utaratibu wa kutoa huduma

Na.	MAELEZO	MUDA
1	Siku za Kazi	Jumatatu - Ijumaa
2	Muda wa kazi	2.00 - 10.00
3	Kujiunga, Kusajili na kukubaliwa Uanachama	Chini ya Siku 14
4	Kukoma Uanachama hadi kurejeshewa Stahiki	Ndani ya Siku 60

5	kufanya mapitio ya Masharti, Sera na Miongozo ya Chama	Miezi 12
6	Kusuluhisha migogoro kati ya Chama na Mwanachma	Siku 60
7	Kuandaa na kuwasilisha makadirio ya mapato na matumizi	Siku 60
8	Kuandaa hesabu za Chama kwa ajili ya kukaguliwa	Siku 90
9	Mkutano Mkuu wa Chama	Miezi 12
10	Mkutano Mkuu wa Kawaida	Miezi 12
11	Mkutano Mkuu Maalum	Itategemea Wanachama/Bodi/ Mrajis
12	Kuhamasisha wanachama kuweka akiba	Kila mara
13	Kutoa mafunzo juu ya Ushirika	Kila mara
14	Kuwachukulia hatua za kinidhamu watumishi wenye makosa	Kila inapotokea
15	Kujibu barua na mawasiliano ya Wanachama	Ndani ya Siku 7
16	Kuhakikisha kuwa orodha ya mishahara ni sahihi	Kila mwezi
17	Kuandaa na kulipa stahili za watumishi	Kila inapotokea
18	kuidhinisha na kutoa mkopo (Dev/Super)	Siku 7
19	Muda wa kuanza kurejesha mkopo *(Grace period)*	Siku 15
20	Kuweka Hisa ya Hiari, Lazima na Akiba	Kila mara

2.4 Ufuatiliaji wa Malalamiko

Malalamiko na mapendekezo ya Wanachama yatachukuliwa kama changamoto na kugeuzwa kuwa fursa na kushughulikiwa haraka iwezekenavyo na Wahusika.

2.5 Jinsi ya kutuma Malalamiko au Mapendekezo

Malalamiko au mapendekezo yanaweza kuwasilishwa, kuwekwa kwenye sanduku la maoni au kutumwa kwa njia ya posta kupitia anuani ifuatayo;

Mwenyekiti wa Chama, S.L.P 76833, Dar es Salaam- Tanzania, simu: +255737583561 Barua pepe: info@lesasaccos.or.tz Web: https://lesasaccos.or.tz

SEHEMU YA TATU

3.0 TAARIFA ZITAKAZOWEKWA WAZI WAKATI WOTE NA CHAMA

Chama kitahakiksha kinatoa taarifa katika maeneo yafuatayo; -

3.1 Taarifa zinazohusu Hisa, Akiba na Amana

Chamakitaweka bayana taarifa zifuatazo kwa maandishi kwa wanachama wake na wanachama tarajiwa zinazohusu hisa, akiba au amana

a) Taarifa ya Akaunti ya hisa, akiba au amana itatolewa kwa mwanachama husika wa akaunti hiyo.

b) Akaunti zinazostahili gawio: Chama kitaweka bayana taarifa za viwango vya gawio vya kipindi kilichopita au kiwango tarajiwa na asilimia ya mapato kwa mwaka. Chama itahakikisha kuwa taarifa zilizowekwa bayana zinaonesha njia iliyotumika kukokotoa malipo ya gawio na itaelezwa wazi kwamba gawio linaweza kutolipwa kama mapato yaliyopo hayatoshelezi au Chama hakijakidhi matakwa ya kisheria.

3.2 Taarifa kuhusu Akaunti zenye Riba

Chama kitatoa taarifa kuhusu kiwango cha riba kilichowekwa na asilimia ya mapato kwa mwaka kama kilivyowekwa na Bodi na njia iliyotumika kukokotoa riba. Aidha, Chama itaeleza bayana kama akaunti ina viwango vya riba vinavyobadilika au visivyobadilika. Taarifa yoyote itakayotolewa kwa ajili ya akaunti za viwango visivyobadilika itajumuisha kipindi cha muda ambapo kiwango hakibadiliki na muda ambapo riba itaanza kuongezeka na wakati malipo ya riba yatakapo iva (*Maturity period*).

Kwa akaunti za viwango vinavyobadilika, taarifa itaeleza yafuatayo: -

a) Uthibitisho kwamba riba inaweza kubadilika;
b) Jinsi riba inavyopatikana;
c) Iwapo kuna alama inayotumika katika kuandaa kiwango kinachobadilika; na
d) Wakati ambapo riba itaanza kuongezeka na viwango vitabadilika.

3.3 Taarifa kuhusu Mabadiliko ya Masharti ya Akaunti

Chama kitatoa notisi ya maandishi kwa wanachama walioathirika na mabadiliko ya akaunti endapo: -

a) Kuna mabadiliko yanapunguza asilimia ya mapato kwa mwaka kwa akaunti za hisa, akiba na amana;
b) Ongezeko la kiwango cha asilimia kwa mwaka cha mikopo, kinaathiri wanachama; au
c) Masharti ya mikopo ya awali, hisa, akiba na amana yanayotambulika yamebadilika.

Notisi iliyotolewa itajumuisha tarehe ya mabadiliko na kutumwa na kupokelewa na whusika angalau siku **thelathini (30**) kabla ya tarehe rasmi ya mabadiliko hayo kuanza kutumika.

3.4 Taarifa ya Kipindi cha Huruma (*Grace period*) cha Kurejesha Mkopo

Chama kitawapatia wakopaji muda wa huruma wa siku kumi na tano (15) katika urejeshaji wa malipo ya mkopo pasipo kutozwa adhabu.

3.5 Taarifa kuhusu Mikopo

Kwa kila muamala wa mkopo, Chama kitaweka wazi masuala yafuatayo: -

a) Kiasi kilichotolewa
b) Gharama za kiasi cha mkopo kilichotolewa ikijumuisha riba na ada
c) Malipo tangulizi ya gharama za fedha zilizokopeshwa; kama yapo
d) Tarehe ambapo gharama za mkopo zitafanyiwa tathmini
e) Gharama nyingine zaidi ya gharama za mkopo
f) Asilimia ya kiwango halisi au kilichowekwa cha riba ya mwaka
g) Kiwango cha ufanisi cha asilimia kwa mwaka kitakachojumuisha gharama za mkopo na ada zote
h) Kiwango cha juu cha asilimia kwa mwaka kinachoweza kutozwa kwa kipindi cha utekelezaji wa masharti ya mkopo
i) Bakaa ya mkopo na njia inayotumika katika ukokotoaji viwango vya riba ili kubaini bakaa ya mkopoambayo kiwango cha riba kimekokotolewa kwa kila kipindi cha malipo

j) Jedwali la malipo likionyesha idadi ya malipo, jumla ya kiasi cha kila malipo, kiasi cha kila malipo ambayo ni ya msingi, riba na ada, na tarehe husika ya kila malipo
k) Jumla ya malipo yote
l) Malipo ya kabla ya adhabu, kama ipo
m) Adhabu ya kuchelewesha malipo
n) Kiwango cha hisa, akiba na amana kinachotakiwa na iwapo fedha hizo zinaweza kutumika kulipia marejesho ya mikopo iliyocheleweshwa.

3.6 Taarifa kuhusu Sababu za Kukataliwa kupewa Mkopo

Endapo maombi ya mkopo yamekataliwa, Chama kitamtaarifu Mkopaji kwa maandishi/barua pepe au simu kuhusu sababu za kukataliwa maombi yake ndani ya masaa ishirini na nne (24) tangu maombi ya mkopo yalipojadiliwa.

3.7 Taarifa kwa Wadhamini wa Mikopo

Chama kitampatia mdhamini taarifa ya maandishi ikionesha wajibu wake kwa mkopo alioudhamini na taarifa hiyo itajumuisha: -

a) Jina na anwani ya Chama
b) Aina ya mkopo
c) Kiasi na tarehe
d) Saini ya mdhamini kama uthibitisho wa kupokea taarifa hiyo.

SEHEMU YA NNE

4.0 Uidhinishwaji wa Sera

Sera hii imetayarishwa na kupitishwa na Bodi ya LESA SACCOS LTD kwa niaba ya wanachama kwa kibali cha Mrajis katika kikao chake kilichofanyika tarehe 17 Julai 2020 na itaanza kutumika baada ya kuidhinishwa na kusajiliwa na Mrajis wa Vyama vya Ushirika.

....
Mwenyekiti

....
Meneja

LESA SAVINGS & CREDIT COOPERATIVE SOCIETY LTD
23 NOV 2020
KINONDONI
DAR ES SALAAM

....
Mrajis wa Vyama vya Ushirika
Tarehe...........................

TANZANIA
Approved this 20TH
day of JANUARY 2021
Asst. Registrar of Cooperative Societies